[A173]

SOMO LA X

# ASILI YA KIROHO NA ASILI YA KIBINADAMU NI TOFAUTI NA YA KIPEKEE

*Makosa ya kawaida ya kutoelewa-Asili ya Kidunia na za Kibinadamu au Asili za Kibingu au Kiroho-Utukufu wa Kidunia na Utukufu wa Kibingu-Ushuhuda wa Biblia Kuhusu Viumbe vya Kiroho-Kinachokufa na Kisichokufa-Je,wanadamu wanaokufa wanaweza kuwa na Uzima wa Milele?-Haki katika Upaji wa Neema-Kanuni Inayodhaniwa Imechunguzwa-Namna nyingi katika Utimilifu-Haki za Mungu za Kifalme-Upaji wa Mungu kwa Mwanadamu ni Sehemu ya Kuridhisha-Uchaguzi wa Mwili wa Kristo-Jinsi Kubadilika kwa Asili Inaathirisha.*

KUKOSA kuona kwamba mpango wa Mungu kwa mwanadamu kwa jumla unazingatia kufanywa upya kwa vitu kama vile vilivyokuwa awali-yaani utimilifu wa binadamu uliopotea pale bustani ya Edeni-na kwamba Kanisa la Wakristo,ambo wako katika mpango huu ,watakuwa na mabadiliko ya asili kutoka asili ya binadamu hadi ya kiroho,Wakristo kawaida wamedhania kwamba hakuna mtu atakayeokoka ila tu wale ambao wamefikia asili ya kiroho.Maandiko,hata hivyo,yakitaja ahadi ya uzima na baraka na kufanywa upya kwa familia zote za dunia,yanatoa na kuahidi mabadiliko ya asili ya kiroho kwa Kanisa pekee ambao wamechaguliwa wakati wa awamu ya Injili;na hakuna fungu hata moja linalopatikana ambalo linadumisha matumaini kama hayo kwa wengine.

Ikiwa umati wa wanadamu wameokolewa kutoka kwa uharibifu,udhaifu,maumivu,taabu na kifo ambavyo vinatokana na dhambi,na wamerudishwa kwa hali ya utimilifu wa mwanadamu ambao ulikuwa kabla ya kuanguka kwa mwanadamu,wameokolewa kabisa kama wale ambao,kwa “mwito mkuu” na wa kipekee wa awamu ya Injili,ambao “watarithi asili ya Kiungu wameokolewa.”

Kukosa kuelewa kile ambacho kinaunda mtu mkamilifu,kukosa kuelewa neno kinachokufa na kisichokufa,na dhana isiyofaa ya haki,zimeleta kosa hili na kufanya maandiko mengi kuwa magumu ambayo yangeeleweka.Ni mtazamo wa kawaida,hata hivyo haujaungwa mkono na fungu lolote la Andiko,kwamba hakuna mtu mkamilifu katika dunia;kwamba vyote tunavyoona vya mwanadamu hapa duniani ni binadamu ambaye hajaendelea na hajakomaa,na kwamba ili afike utimilifu,lazima abadilike awe mwanadamu wa kiroho.Mtazamo huu unaleta kuchangayikiwa kwa Maandiko badala ya kuimarisha maelewano na uzuri unaoletwa na “kutumia neno la ukweli vizuri.”

Maandiko yanafundisha kwamba,kulikuwako na wawili,na walikuwa wawili pekee,ambao walikuwa wakamilifu-Adamu na Yesu.Adamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu:yaani kwa

nguvu za kiakili ya kutoa hoja,kumbukumbu,hukumu na mapenzi,na sifa za haki,ukarimu,upendo n.k. “Kwa dunia,kidunia,” alikuwa mtu wa mfano wa kidunia ya mwanadamu wa kiroho,akiwa na tabia zinazofanana,hata kama zilikuwa tofauti kwa kiwango,upana na upeo.Kwa kiwango hicho mwanadamu bado ni mfano wa Mungu ambao Mungu anaweza kusema kwamba ameanguka, “Njooni tusemezane.”

Kama vile Yehova ndiye mtawala wa vitu vyote,basi mwanadamu aliumbwa kuwa mtawala wa vitu vya kidunia-Kwa mfano wetu,na awe  na mamlaka juu ya hayawani,ndege,samaki,n.k. (***Mwanzo 1:26***).Musa anatuambia (***Mwanzo 1:31***) kwamba Mungu alitambua mwanadamu aliyeumba-sio kwamba alianza tu kuumba lakini alifanya kwa ukamilifu-na Mungu akamwona uumbaji wake kuwa “mzuri kabisa,” yaani,mkamilifu;kwa sababu machoni pa Mungu hakuna kitu kizuri kama sio kikamilifu,katika viumbe vyake vyenye akili.

Ukamilifu wa mwanadamu kama alivyoaumbwa,umeelezwa katika ***Zaburi 8:5-8***: “Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu;Umemvika taji ya utukufu na heshima;Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako;Umevitia vitu vyote chini ya miguu yake.Kondoo,na ng’ombe wote pia;Naam,na wanyama wa kondeni;Ndege wa angani,samaki wa baharini;Na kila kipitacho njia za baharini.” Imependekezwa na wengine ambao wanataka Biblia iendane kulingana na nadharia ya mageuzi,kwamba neno “mdogo,” katika ***Webrania 2:7***,linaweza kueleweka likiwa na maana ya alikuwa mdogo kwa wakati,na siyo kwamba alikuwa mdogo kwa kiwango kuliko malaika.Hata hivyo,hakuna mamlaka wala sababu ya tafsiri hiyo.Hii ni nukuu kutoka kwa ***Zaburi 8:5***,na ulinganifu muhimu wa maandiko ya Kiebrania na Kiyunani yanaweza kufutilia mbali shaka kwa dhana hiyo iliyoagizwa.Dhana hiyo,inaeleza waziwazi  kwamba alifanyiwa mdogo kwa kiwango kuliko malaika.

Daudi,katika Zaburi,anatoa maelezo kwa mwanadamu katika hali yake ya awali,na anadokeza kwamba Mungu  hakuuwacha mpango wake wa awali wa kumwacha katika sura yake na kuwa mfalme wa dunia,na kwamba atamkumbuka,kumkomboa na kumrejesha ufalme tena.Mtume (***Waeb.2:7***) anatukumbusha ukweli huo-kwamba kusudi la Mungu la awali halikuachwa;kwamba mwanadamu aliyekuwa mfalme mkamilifu na mtimilifu,atakumbukwa na kutembelewa,na kurejeshwa.Anaongeza,Hatujaona ahadi ya kufanywa upya bado lakini tunaona hatua ya kwanza Mungu ameichukuwa ili apate kuikamilisha.Twaona Yesu amewekewa taji ya utukufu na heshima ya mtu mkamilifu,kwamba yeye,aliyehitimu kuwa fidia au  mbadala aweze kuonja mauti kwa neema kwa ajili ya watu wote,ili apate kutengeneza njia ya uwekeaji upya wa mwanadamu kwa yale yote yaliyopotea.Rotherman,mmoja wa watafsiri wa ajabu sana,anaeleza kifungu hiki kama ifuatavyo:

"Mwanadamu ni nini  hata umkumbuke;
Ama mwana wa binadamu,hata umwangalie?
Umemfanya mdogo punde kuliko malaika:
Umemvika taji ya utukufu na heshima,
Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako."

Haipaswi kuonekana kwamba kumfanya mdogo katika kiwango inamaanisha kwamba alifanywa mdogo kwa ukamilifu.Kiumbe kinaweza kuwa mkamilifu,japo kwa kiwango cha chini kuliko

mwingine;kama vile,farasi mkamilifu [A176] yuawezakuwa wa kiwango cha chini kuliko mwanadamu,n.k.Kuna asili tofauti,wachangamfu na wasio wachangamfu.Kwa kueleza,tunapanga yafuatayo katika jedwali:

**Viwango vya Kibingu au Mwanadamu wa Kiroho**

Malaika

Viwango vya Kidunia au Binadamu mnyama

Binadamu

Hayawani

Nyuni

Samaki

Viwango katika Uwanja wa Mboga

Miti

Vichaka

Nyasi

Kuvumwani

Viwango katika Uwanja wa Madini

Dhahabu

Fedha

Shaba

Chuma

Kila moja ya madini yaliyotajwa yanaweza kuwa safi.lakini dhahabu yanakuwa safi zaidi.Ingawa kila kiwango cha miti kinapaswa kiletwe kwa ukamilifu,bado watatofautiana katika asili na cheo.Vivyo hivyo na Wanyama,ikiwa aina ya wanyama wanaletwa kwa ukamilifu,bado kutakuwa aina mbalimbali,kwa sababu kumweka aina haibadilishi asili yake.Viwango vya viumbe vya kiroho,pia,hata kama ni mkamilifu,wanahuasiana kila mmoja wanakuwa katika kiwango cha chini katika asili na aina.Asili ya kiungu ndiyo ya kiwango cha juu na bora kwa asili zote za kiroho.Kristo katika kufufuka kwake "*alifanywa bora sana*" kuliko malaika wakamilifu wote kwa sababu asili ya kiungu ni bora kuliko asili ya kimalaika *Waeb. 1:3-5*

**Wakati mwingine neno asili hutumika katika hali ya hisani,kama,kwa mfano,ikisemekana kwamba mbwa asili yake ni ukali,ama farasi ana asili ya upole,ama tabia mbaya.Lakini kwa kutumia neno hilo basi linaonyesha*

*uchambuzi tu wa yule anayeelezwa akilinganishwa na wengine,lakini halionyeshi asili kamili ya huyo mnyama..*

---

Kumbuka kwa makini kwamba viwango ambavo vimetajwa hapa juu kwenye orodha ni tofauti na vinatengana.japo kuna ulinganifu kati yao waweza kuonekana,hivyo:Kiwango cha juu ya madini ni duni au cha chini kuliko kiwango cha chini cha mboga,kwa sababu kwa mboga kuna uhai.Kwa hiyo kiwango cha chini ya mboga kiko chini kuliko kiwango cha chini cha mnyama,kwa sababu mnyama ana uhai,na hata katika kiwango chake cha chini,ana akili ya kutosha kuwa na ufahamu ya kuwepo.Vivyo hivyo,mwanadamu,japo ni mnyama wa kiwango cha juu katika wanyama wote wa kidunia au viumbe vya dunia,ni “mdogo kuliko malaika,” kwa sababu malaika ni viumbe vya kiroho au vya kibingu.

Twaona tofauti kubwa kati ya mwanadamu kama vile tunavyomwona sasa,ambaye amepungukiwa kwa ajili ya dhambi,na mwanadamu aliyekuwa mkamilifu ambaye Mungu aliumba kwa sura yake.Dhambi imebadili sura yake,na tabia zake.Vizazi vingi vilivyozidi,kwa kutojali,kwa kuruhusu na kunyimwa kwa kawaida,wameharibu na kuvunja sura ya binadamu kiasi cha kwamba kizazi kikubwa cha binadamu kimeharibu mfano wa sura ya Mungu.Sifa za kimaadili na kiakili zimeharibika;na silka ya mnyama,ambayo haijawahi kuendelea haiwezi kuwekwa sana na wale walio wa juu.Mwanadamu amepoteza nguvu za kawaida kiasi kwamba pamoja na sayansi yote ya matibabu,upana wa uhai wake ni karibia miaka thelathini,ilhali hapo mwanzo alikuwa akiishi miaka mia tisa na thelathini chini ya adhabu sawa.Hata kama amenajisiwa na kuaibishwa na dhambi na adhabu yake,kifo,ambacho kinafanya kazi ndani yake,mwanadamu atarudishwa kwa ukamilifu wake wa awali wa mawazo na mwili,na utukufu,heshima na utawala,kwa wakati na kwa utawala wa miaka elfu wa Kristo.Vitu ambavyo vitarejeshwa ni vile ambavyo vilipotea kupitia kwa uasi wa Adamu. (***Warumi 5:18,19***).Mwanadamu hakupoteza paradiso wa Mbinguni lakini alipoteza Paradiso wa kidunia.Chini ya adhabu ya mauti,hakupoteza uwepo wa kiroho lakini alipoteza uwepo wa kibinadamu;na yale yote yaliyopotea yalikombolewa tena na Mkombozi wa mwanadamu,ambaye alitangaza kwamba alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea.. *Luka 19:10*

Pamoja na hayo ya juu,tuna uthibitisho kwamba mtu mkamilifu siye kiumbe cha kiroho.Twaambiwa kwamba,Bwana wetu,kabla hajaacha utukufu ili awe binadamu,alikuwa “mfano wa Mungu”-mfano wa binadamu,kiumbe cha kiroho;kwa vile ili awe fidia kwa wanadamu angekuwa mwanadamu,ya asili sawa na mwenye dhambi ambaye lazima angepitia kifo,ingebidi kwamba asili yake ibadilishwe.Na Paulo anatueleza kwamba alichukua asili ya malaika,hatua moja chini ya asili yake,na kuja chini hatua mbili na kuchukua asili ya wanadamu-akawa mwanadamu;basi, “akafanywa mwili ." *Waeb. 2:16*; *Wafilipi 2:7,8*; *Yohana 1:14*

Kumbuka kwamba jambo hili linatufunza kwamba sio asili ya kimalaika ndiyo inapatikana katika asili ya kiroho pekee,lakini kwamba malaika wana asili ambayo iko chini kuliko ile ya Bwana kabla hajakuwa mwanadamu;na hakuwa juu kama vile alivyo sasa,kwa sababu, “ Mungu

amemtukuza sana.” Kwa sababu ya kutii kwake ili awe fidia kwa wanadamu.(***Wafilipi 2:8,9***).Sasa amekuwa katika ngazi ya juu sana ya kiumbe cha roho,akichukua asili takatifu ya Yehova.

Lakini siyo kwamba twapata uthibitisho kwamba asili takatifu,za kimalaika na za kibinadamu zimekuwa zikitengana na tofauti,basi jambo hili linathibitisha kwamba mtu mkamilifu siyo kubadilika uwe kama malaika,zaidi na ukamilifu wa asili ya malaika unaonyesha kwamba malaika ni watakatifu kama Yehova;kwa sababu Yesu hakuchukuwa asili ya malaika,lakini asili tofauti-asili ya wanadamu;sio asili isiyo kamilifu wa mwanadamu kama vile tunavyomiliki,lakini asili kamilifu ya mwanadamu.Alikuwa mwanadamu;sio wenye aibu na kiumbe ambacho kinakaribia kufa kama wanadamu walivyo sasa,lakini mwanadamu aliyekuwa katika nguvu ya ukamilifu.

Na tena,Yesu lazima angekuwa binadamu mkamilifu la sivyo hangetunza amri takatifu,ambayo inaonyesha kiwango kamili ya uwezo mkamilifu wa mwanadamu.Na lazima angekuwa mtu mkamilifu la sivyo hangeweza kujitoa kama fidia ( gharama iliyotosha-***1 Timotheo 2:6***) kwa sababu kwa kuacha maisha kamilifu ya Adamu; “Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu,kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu..” (***1 Wakorintho 15:21***).Kama angekuwa kwa kiwango cha kukosa ukamilifu,basi ingethibitishwa kwamba alikuwa chini ya hukumu,na basi angekubalika kuwa dhabihu bora,na hata hangeweza kutunza amri za Mungu kwa ukamilifu.Mtu mkamilifu alijaribiwa na hakufaulu,na akahukumiwa,kwa hivyo mtu mtimilifu ndiye angetoa gharama ya Mkombozi.

Basi tunalo swali mbele yetu katika njia nyingine, km:Ikiwa Yesu katika mwili alikuwa mtu mtimilifu,kama vile Maandiko yanavyoonyesha,je,haithibitishi kwamba mtu mtimilifu ni binadamu,kiumbe chenye mwili-sio malaika,lakini yuko chini kidogo kwa malaika? Hitimisho la kimaantiki halina kosa;na kwa kuongeza tuna maelezo yaliyotiwa msukumo na Mwandishi wa Zaburi ( ***Zaburi 8:5-8***) na marejeo ya Paulo katika *Waeb. 2:7-9*.

Yesu hakuwa mchanganyiko wa asili mbili,yaani ya binadamu na ya kiroho.Kuchanganywa kwa asili mbili hakuleti asili ya kiroho au ya kibinadamu,lakini kunaleta mseto usio kamili ambao haujisiki kwa mpangilio wa Mungu.Wakati Yesu alikuwa katika mwili alikuwa kiumbe kamilifu cha kibinadamu; kabla ya kuwa katika mwili,alikuwa kiumbe kamilifu cha kiroho;na baada ya ufufuo wake,amerudi kuwa kiumbe kamilifu wa kiroho wa ngazi ya juu sana wa kiungu.Alipata hakikisho la kuwa kiumbe kamilifu wa kiroho wakati wa kuwekwa kwake wakfu hata mpaka wakati wa kifo chake,kama ilivyoonyeshwa na ubatiso-akiwa miaka thelathini (akiwa binadamu,kulingana na Sheria,na akiwa na umri mzuri wa kuwekwa wakfu kwa mwanamume)-ambapo alipokea haki ya kuwa kiumbe cha kiroho. (***Mathayo 3:16,17***).Asili ya kibinadamu ingewekwa wakfu kwa mauti kabla hajapokea hata ahadi ya kuwa kiumbe takatifu.Na ilifanyika wakati wa kuwekwa wakfu ambapo alibebwa na kujitoa kama dhabihu ili amalize asili ya kibinadamu,hadi mpaka kifo,ambapo Bwana wetu Yesu alikuwa mshiriki wa asili ya kiroho. (***Wafilipi 2:8,9***).Ikiwa andiko hili ni la kweli,linaeleza kwamba hakutukuzwa kuwa na asili ya kiumbe takatifu hadi asili ya binadamu ilipotolewa kama dhabihu-kupitia kifo.

Kwa hiyo twaona kwamba kwa Yesu hakukuwa na mchangayiko wa asili,lakini ukweli ni kwamba alipata kubadilisha asili;kwanza kutoka kwa kiroho hadi kwa binadamu;baadaye kutoka kwa mwanadamu hadi kwa kiwango kikuu cha kiroho,takatifu;na kwa kila hali moja iliachwa kwa ajili ya mwingine.

Katika mfano huu mwanana wa uanadamu mkamilifu,ambaye hakupatikana na kasoro mbele ya ulimwengu hadi wakati aliposulubishwa kwa ukombozi wa ulimwengu,twaona utimilifu ambao kizazi chetu walianguka kupitia kwa Adamu,na ambapo atakaporejeshewa.Kwa kuwa fidia kwa wanadamu,Bwana wetu Yesu Kristo alitoa kile kilichoambatana na wanadamu walichokipoteza;na kwa hivyo,wanadamu wote wanaweza kupata tena,kupitia kwa Imani katika Kristo,na kuutii maelezo yake kwa mahitaji yake,siyo wa kiroho lakini asili takatifu-kwa " kile ambacho kilipotea."

Sehemu za mwanadamu kamili na nguvu zake zaweza kutumika kwa muda usiojulikana,na kwa vifaa vinavyohitajika,na maarifa na ujuzi vinaweza kuongezeka;lakini kuongezeka kwa maarifa na nguvu hakuwezi kuathiri kubadilika kwa asili,ama kuifanya iwe kamilifu sana.Itakuwa tu kupanuka na kuendelea kwa nguvu kamili ya mwanadamu.Kuongezeka kwa maarifa na ujuzi bila shaka itakuwa haki kwa wote milele;japo bado hatakuwa ni mwanadamu,na atakuwa tu akijaribu kujifunza jinsi ya kutumia nguvu zote za asili za mwanadamu ambazo amemiliki.Zaidi ya uwezo wake hawezi kutumainia,ama kutamani,mapema nguvu ambayo imezidi uwezo wake.

Wakati Yesu kama mtu alikuwa onyesho la asili ya mwanadamu mkamilifu.ambaye umati wa watu watarejeshwa,japo tangia ufufuo wake amekuwa mfano wa asili tukufu ambayo Kanisa linaloshinda,wakati wa ufufuo,watashiriki kwaye.

Kwa sababu awamu hii ya sasa imetengwa hasa kwa kukuza darasa hili ambalo limetolewa kwa kubadilishwa kwa asili,na kwa sababu barua za kitume zimetengwa kwa agizo hili la " kundi dogo," haipaswi kuonekana kwamba mpango wa Mungu unaisha kwa kukamilika kwa kundi hili lililochaguliwa.Na pia,kwamba twaweza kuangalia kinyume chake,na kudokeza kwamba ahadi za kipekee ya asili ya utukufu,miili ya kiroho,n.k., iliyofanywa kwa ajili hiyo,na mpango wa Mungu kwa wanadamu wote.Kwa hawa wote " ametukirimia ahadi kubwa mno," kwa ajili ya watu wote.Kwa kutumia Neno la ukweli,twapaswa kuangalia kwamba Maandiko yanatambua utimilifu wa asili tukufu kwa "kundi dogo," na utimilifu wa asili ya mwanadamu katika ulimwengu utakaorejeshwa,kama vitu viwili tofauti.

Wacha tuangalie kwa kina hasa,Ni nini maana ya viumbe vya kiroho? Nguvu zao ni gani? Na wanatumia sheria gani? Wengi wanadhani kwamba asili ya kiroho ni Imani potofu,na kwa suala hili itikadi ya kudhaniwa inashinda.Lakini Paulo anaonekana kwamba hana dhana hiyo.Ingawa yeye anasisitiza kwamba mwanadamu hawezi kuelewa hali ya juu ya kiroho ( ***1 Wakorintho 2:14)***,japo anasema waziwazi ,kana kwamba analinda dhidi ya nadharia na mawazo ya kidini,kwamba kuna mwili wa kiroho,pamoja na mwili wa asili wa kibinadamu,kama vile dunia na utukufu wa kidunia na pia utukufu wa kibingu.Utukufu wa kidunia,kama vile tumeona,ulipotezwa na dhambi ya Adamu wa kwanza,na utarejeshwa kwa mbari na Bwana Yesu na Mkewe (Kristo,Kichwa na mwili) wakati wa utawala wa miaka elfu moja.Utukufu wa kibingu haujaoonekana lakini umefunuliwa kwa jicho la Imani na Roho kupitia kwa

Neno.Utukufu huo ni tofauti na unatengana.(*1 Wakorintho 15:38-49*) Twajua kiasi kwamba mwili huu wa kawaida,wa kidunia utakuwa mkamilifu kama vile tunavyokadiria.Ni nyama,damu na mifupa;kwa sababu "kilichozaliwa na mwili ni mwili." Na kwa sababu ni aina mbili za miili tofauti,twajua kwamba mwili wa kiroho,kwa vyovyote vile,hauna nyama,damu na mifupa:ni mwili wa kibingu,na wa kiroho-" Aliyezaliwa na Roho ni roho."Lakini mwili wa kiroho unafanana,hatujui,kwa sababu "Hatujajua vile tutakavyokuwa;lakini…tutakuwa kama yeye"-kama Bwana wetu Yesu Kristo . *Yohana 3:6*; *1 Yohana 3:2*

Hatuna rekodi yoyote wa binadamu ,kwa njia ya mwili au kiroho,amebadilishwa kutoka kwa asili moja hadi asili nyingine,ila tu Mwana wa Mungu;na huyu alifanyiwa kwa njia ya kipekee,kwa kusudi la kipekee.Wakati Mungu aliwaumba malaika,aliwaumba wawe malaika milele,na pia wanadamu waliumbwa wawe wanadamu,kila mmoja kwa njia yake ya ukamilifu.Angalau Maandiko hayatoi maelezo ya kusudi tofauti.Kama ilivyo katika uumbaji usio wa kawaida kuna aina ya kupendeza na isiyo na mwisho,kwa hiyo katika viumbe hai na vya akili,aina sawa ya ukamilifu inawezekana.Kila kiumbe katika ukamilifu wake ni tukufu;lakini kama vile Paulo anavyosema,utukufu wa kibingu ni mojawapo wa utukufu,na utukufu wa kidunia ni utukufu tofauti.

Kwa kuchunguza ukweli ulioandikwa wa Bwana Yesu Kristo baada ya kufufuka kwake,na wa malaika,ambao pia ni viumbe vya kiroho,basi "tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni." (*1 Wakorintho 2:13*),twaweza kupata maelezo ya jumla kuhusu viumbe vya roho.Kwanza,malaika wa wanaweza kuwepo na mara nyingi wanakuwepo,lakini hawaonekani. "Malaika wa BWANA hufanya kitu,akiwazunguka wamchao na kuwaokoa." " Je! Hao wote si roho watumikao,wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu?" (*Zaburi 34:7;Waeb.1:14*).Je! Wamehudumu wakionekana au wasipoonekana? Hasa wanahudumu wasipoonekana.Elisha alizungukwa na washuru wengi;mtumishi wake aliogopa;Elisha aliomba Bwana,na macho ya kijana huyo yakafunguliwa, na akaona milima karibu nao ikijaa na magari ya moto na wapanda farasi wa moto ( au kama moto).Pia,wakati kwa Balaamu malaika hakuonekana,punda alipofunguliwa macho,alipata kuona huyo malaika.

Ya pili,malaika wanaweza kuwa na miili ya wanadamu na kuonekana na watu.Bwana na malaika wawili walionekana na Ibrahimu,ambaye aliwatengenezea chakula cha jioni,ambacho walikula. Mara ya kwanza Ibrahimu alidhani kuwa walikuwa watu watatu,na alitambua baadaye kwamba mmoja alikuwa Bwana na wawili walikuwa malaika,ambao baadaye walienda Sodoma na kuokoa Lutu. (*Mwanzo 18:18:1,2*) Malaika alionekana na Gedioni kama mwanadamu,lakini baadaye alijitambulisha.Malaika alionekana na babake na mamake Samson,na walidhani kwamba ni mtu hadi wakati alipopaa mbinguni katika moto wa madhabahu.*Waamuzi 6:11-22; 13:20*

Ya tatu,viumbe vya kiroho wana utukufu katika hali yao ya kawaida,na mara nyingi wanajulikana kama wenye utukufu na mwanga.Uso wa malaika ambaye alivingirisha jiwe kutoka kwa mlango wa kaburi ulikuwa "kama umeme".Danieli alipata kuona mwili wa kiroho,ambaye alieleza ,akisema,macho yake yalikuwa kama taa za moto,na sura yake kama umeme,mikono na miguu yake kama rangi ya shaba iliyopigwa,na sauti yake kama sauti ya umati.Danieli alianguka mbele yake kama bubu.(*Dan.10:6,10,15,17*).Saulo wa Tarso alipata ya

mwili wa utukufu wa Kristo ulioonekana juu ya mwangaza wa jua wakati wa mchana.Saulo alipoteza macho yake na akaanguka chini.

Kwa hivyo tumepata kwamba viumbe vya kiroho kwa kweli wana utukufu;isipokuwa kwa kufunguliwa kwa macho ya watu twaweza kuwaona,ama wakionekana katika mwili kama watu,kwa sababu hawaonekani kwa urahisi na watu.Hitimisho hili linathibitishwa zaidi wakati tunachunguza maelezo fulani ya maonyesho haya.Bwana alionekana na Sauli pekee,watu waliotembea na yeye,walisikia sauti lakini hawakumwona mtu ye yote. (***Matendo 9:7***) Watu waliokuwa na Danieli hawakuona kiumbe mwenye utukufu ambaye alieleza,lakini wakajawa na hofu,na wakakimbia na kujificha.Tena,kiumbe mwenye utukufu huyo alitangaza, "Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alinipinga siku ishirini na moja." (***Dan.10:13***).Je,Danieli,mtu ambaye alipendwa sana na Bwana,alianguka kama mfu mbele ya yule ambaye mfalme wa Uajemi alipinga kwa siku ishirini na moja? Je,ilikuwaje? Kwa ukweli hakuonekana katika utukufu wa mfalme! Yuaweza kuwa alionekana kwa njia nyingine tofauti au alionekana kama mwanadamu.

Bwana wetu,tangia wakati alifufuka,amekuwa kiumbe wa kiroho;pia nguvu tunazopata ambazo zimeelezwa kwa malaika (viumbe vya kiroho) ni nguvu ambazo anapaswa kuwa nazo.Na hivyo ndivyo itakavyokuwa kama vile tutakavyoona katika sura inayofuata.

Kwa hivyo tumepata kwamba Maandiko yanaonyesha kwamba asili ya kiroho na ya kibinadamu ni tofauti na zinatengana,na hayana uthibitisho kwamba mtu atageuka au kuwa katika kiumbe kingine,lakini kinyume ni kwamba yanatuonyesha kuwa wachache watabadilishwa toka kwa binadamu hadi kwa asili takatifu,ambayo Yesu,kichwa chao,tayari ametukuzwa kuwa katika utukufu.Na sifa hii ya kushangaza na maalum katika mpango wa Yehova ni kwa kusudi la kushangaza na maalum ya kuwandaa kama mawakala wa Mungu kwa kazi kuu zijazo ya kufanya upya vitu vyote.

Wacha basi tuchunguze sasa maneno.

**Kinachokufa na Kisichokufa.**

Tutapata umuhimu wao wa kweli kwa maelewano halisi na yale tuliyojifunza kutokana na kulinganisha kwa maneno ya Biblia kuhusu viumbe wa kibinadamu na wa kiroho,na ahadi za kidunia na za mbinguni.Maneno haya kwa kawaida hutolewa maana isiyo na uhakika,na mawazo mabaya ya maana yao huzalisha dhana potofu ya masomo ambayo wanasimama kushikamana,kwa ujumla na katika matumizi ya kimaandiko.

"*Kinachokufa*" inaonyesha hali ya uwezekano wa kufa,sio lazima kifo bali ni hali ambayo kuna uwezekano.

"*Kisichokufa*" inaonyesha hali ya kutoweza kufa;si hali tu ya kuwa na uhuru wa kutokufa,bali ni hali ambayo kuna uwezekano kutokufa.

Dhana ya kawaida lakini ya uongo ni kwamba kinachokufa ni hali ambayo mauti hauwezi kuepukana kwayo,wakati dhana kawaida ya kutokufa inaleta maana.

Neno *kisichokufa* linaonyesha kile kisichoweza kufa;kwa hivyo muundo wa maneno hayo unaonyesha maana yao kamili.Ni kwa sababu ya dhana ya uongo ya neno kinachokufa ambapo

wengi sana walichanganyikiwa wakijaribu kutambua ikiwa Adamu alikuwa mtu anayeweza kufa au asiyeweza kufa kabla hajafanya dhambi. Wanasema kwamba ikiwa alikuwa mtu asiyeweza kufa Mungu angesema, “Siku ile atakayekula basi hakika atakufa”; kwa sababu aliye na uhai wa milele hawezi kufa.Hii ni hitimisho la kimantiki.Kwa njia nyingine,twasema,angekuwa mtu wa kufa,basi kungetokea wapi tishio au adhabu ya maelezo haya, “Hakika atakufa” ; kwa vile ikiwa kinachoweza kufa (kulingana na ufafanuzi wao usio sahihi) hangeweza kuepuka kifo hata hivyo?

Ugumu ambao utatokea utakuwa katika maana isiyo sahihi iliopeanwa ya neno *kinachokufa*.Ukitumia ufafanuzi sahihi basi yote yatakuwa wazi.Adamu alikuwa mtu wa kufa- hiyo ina maana kwamba alikuwa katika hali ambayo kifo kingewezekana.Alikuwa na maisha kwa kipimo kamili na kamilifu,lakini si uhai wa asili.Ilikuwa ni maisha ya kudumishwa na “ kila mti wa bustani” ila mti mmoja iliozuiliwa,na kwa muda mrefu alipokuwa akiendelea kwa kutii kwa mujibu wa Muumba wake,maisha yake yalikuwa na vipengele vya kudumisha salama ambavyo havikataliwi.Hta hivyo,vile inavyoonekana,Adamu alikuwa na uhai,na mauti ungeepushwa,japo alikuwa katika hali ambapo kifo kingewezekana-yaani alikuwa mtu anayeweza kufa.

Swali linatokea,basi,kama Adamu alikuwa mtu wa kufa na wa kupitia jaribio,je,alikuwa kwenye jaribio la kutokufa? Kawaida jibu litakuwa Ndiyo.Lakini twajibu ,Hapana.Jaribio lake lilikuwa ni kuona kama alikuwa anastahili au hastahili kuendelea na maisha na baraka zilizokuwa zimemilikiwa.Kwa sababu hakuna mahali popote aliahidiwa kwamba ikiwa atakuwa mtiifu basi atakuwa mtu asiyeweza kufa,twapaswa kuondoa visio vyote nje ya swali.Aliahidiwa kuendelea kwa baraka kisha akafurahia muda mrefu kama mtiifu,na kutishiwa na kupoteza kwa yote- kupitia kwa-ikiwa amekosa kutii.Ni dhana ya uongo la maana ya neno kinachokufa ndilo linaongoza watu kwa ujumla kuhitimisha kwamba viumbe vyote ambao hawafi ni wa kudumu milele.Katika kitengo hiki,wanajumuisha Baba wetu wa mbinguni,Bwana wetu Yesu,malaika,na wanadamu wote.Hili wazo basi ni uongo,halaiki kubwa ya watu waliookolewa kutoka kwa mwanguko,pamoja na malaika wa mbinguni,watazidi kuwa chini ya kifo;japo kwa hali ya utimilifu na furaha,watazidi kuwa na asili ya kufa ambao wanaweza kufa,mshahara wa dhambi ambao wanapata kwa kutenda dhambi.Usalama wa kuwepo kwao utawekwa,kama ilivyowekewa Adamu kwa kumtii Mungu mwenye hekima,na nguzu za kufanya kazi kwa ajili ya mema kwa wale wanaompenda na kumtumikia,watakuwa wameoshwa kikamilifu na matendo yake dhambi kwa wakati huu.

Hakuna mahali popote katika Maandiko yametajwa kwamba malaika hawafi,na pia kwamba wanadamu waliofanywa upya hawatakufa.Kinyume cha hayo,kutokufa kumeachiwa asili ya kiungu pekee-hasa kwa Yehova pekee;na pia kwa Bwana wetu Yesu katika hali yake ya sasa iliyoinuliwa sana;na hatimaye kwa Kanisa lilioahidiwa,yaani mwili wa Kristo,watakapotukuzwa na yeye.. *1 Tim. 6:16*; *Yohana 5:26*; *2 Pet. 1:4*; *1 Wakor. 15:53,54*

Sio tu kwamba tuna ushahidi kuwa kutokufa huhusu tu asili ya Mungu,lakini tuna ushahidi kwamba malaika anaweza kufa,kwa kweli Shetani ambaye alikuwa mkuu wa idadi yao,ataharibiwa.(***Waeb.2:14***).Ukweli kwamba wataharibiwa unathibitisha kwamba malaika kwa kitengo chao wanaweza kufa.

Kwa hiyo tukiangalia,twaona kwamba wakati wenye dhambi wasioweza kurekebishwa wameondolewa,wanadamu wasioweza kufa na wanaoweza kufa wataishi milele kwa furaha na upendo-kitengo cha kwanza ambacho wana uwezo wa kutokufa,wanao uhai ndani yao (***Yohana 5:26***);.na wa mwisho wakiwa na asili inayoathiriwa na kifo,japo kwa sababu ya ukamilifu wao na maarifa ya uovu na uovu wa dhambi,na kutotoa sababu ya mauti.Wao,kwa sababu watathibitishwa na sheria ya Mungu,watapewa mambo hayo muhimu yanayoweza kuwasaidia katika utimilifu,na hawataweza kufa kamwe.

Utambuzi unaofaa wa maana ya maneno kufa na kutokufa,na matumizi yao katika Maandiko,unaharibu msingi wa fundisho la adhabu ya milele.Fundisho hilo limejengwa juu ya nadharia yasiyo ya maandiko kwamba Mungu alimwumba mtu asiyeweza kufa,kwamba hawezi kukosa kuwepo,na kwamba Mungu hawezi kumharibu;na hivyo ndivyo mabishano kwamba watu wasioweza kutubu lazima waendelee kuishi sehemu fulani na kwa jinsi fulani,na hitimisho ni kwamba kwa vile hawaendi pamoja na Mungu basi hatima yao lazima iwe ya taabu.Lakini neno la Mungu linatuhakikishia kwamba amewapa dhidi ya uendelezaji wa dhambi na wenye dhambi:kwamba mtu anakufa,na kwamba adhabu ya kutosha ya kutenda dhambi kwa makusudi dhidi ya nuru na maarifa haitakuwa kuteseka katika adhabu ya milele,lakini itakuwa ni mauti ya pili. “Roho itendayo dhambi,itakufa.”

**"Wewe U Nani Umjibuye Mungu?"**
*Warumi 9:20*

Ni dhana ya kimakosa ya baadhi ya watu kwamba haki inahitaji kuwa Mungu asiweke tofauti yoyote katika kutoa neema zake miongoni mwa viumbe vyake;kwamba ikiwa ameinua mmoja kwa nafasi ya juu,katika haki lazima afanye hivyo kwa wote,isipokuwa inaweza kuonyeshwa kuwa wengine wamepoteza haki zao,katika hali hiyo anaweza kupewa nafasi ya chini kulingana na haki.

Ikiwa kanuni hii ni sahihi,basi itaonyesha kwamba Mungu hana haki ya kumwumba Yesu kuwa juu ya malaika,na pia kumwinua juu kwa asili ya kiungu,ila tu kama alikusudia kuwafanyia malaika wote na watu wote hivyo.Na kwa kuendeleza kanuni hii kwa kina,ikiwa watu wengine wanaweza kutukuzwa na kumiliki asili ya kiungu,watu wote basi hatimaye watainuliwa kwa nafasi hiyo.Na kwa nini kanuni hii isiendelezwe kwa kiwango chake cha juu,na kutumia sheria ya undelezaji wa uumbaji wa wanyama na wadudu,na kusema kwamba kwa sababu wote ni viumbe vya Mungu basi lazima wote wafikie kiwango cha juu sana ya uwepo-yaani ya asili ya kiungu? Huu ni upotofu wa wazi,lakini kuna upungufu mwingine wa kanuni hii inayodhaniwa.

Pengine hakuna mtu anayeweza kubeba dhana ya uongo hadi sasa.Hata hivyo kama ilikuwa kanuni iliyoanzishwa katika haki,ingekwama wapi na bado iweze kuwa wa haki? Na ikiwa huo ndio ulikuwa mpango wa Mungu,basi wapi aina tofauti ya kazi zake zote zinazopendeza? Lakini huo sio mpango wa Mungu.Asili zote,.wanaochamsha na wasiochangamsha,wanaonyesha utukufu na tofauti za nguvu na hekima ya kiungu.Na kama vile “mbingu zinatangaza utukufu wa Mungu,na anga inaonyesha kazi ya mikono yake” katika vitu vingi na uzuri,basi hata uumbaji wake wenye hekima wanaonyesha katika njia tofauti utukufu wa hali ya juu ya nguvu yake.Kwa

hivyo tunahitimisha kutoka kwa mafundisho la Neno la Mungu,kutoka kwa wazo na kutoka kwa mifano ya asili.

Ni muhimu sana tukiwa na dhana sahihi ya haki.Neema haipaswi kutukuzwa  kama fidia inayostahili haki.Tendo rahisi la haki wakati mwingine halionyeshi shukrani maalum,wala si ushahidi wowote wa upendo;lakini Mungu anaonyesha upendo wake mkubwa kwa viumbe vyake,katika ngazi ya milele ya  neema isiyostahili,ambayo inahitaji upendo wake na kushukuru kutoka kwetu.

Mungu ana haki,ikiwa anataka,ya kufanya viumbe tu wa kuchukua muda mfupi,hata kama hatukutenda dhambi.Kwa hiyo ameviumba viumbe wengine katika ngazi ya chini.Angeruhusu tufurahie baraka zake kwa muda tu,kisha baadaye,bila haki,angetumaliza ili tusizidi kuwepo.Hakika,hata kuwepo kwetu kwa muda bado kungekuwa neema.Ni kwa neema tu ndiyo sisi sote tunapata kuwepo.Ni neema kiasi gani imeonyeshwa na ukombozi wa kuwepo kwetu ambayo ilipotezwa kwa ajili ya dhambi! Zaidi ya hayo,ni kwa kupitia kwa neema ya Mungu tumefanywa wanadamu wala sio wanyama,ni neema bure ya Mungu iliyofanya malaika kuumbwa na asili ambayo iko juu ya wanadamu;na pia ni kwa neema ya Mungu tunapata kwamba Bwana Yesu na Bi harusi wake wakawa washiriki wa asili ya utukufu.Wote wamekuwa viumbe wenye akili,ili kwamba wapokee shukrani kwa kile ambacho Mungu amefanya.Roho mwingine yeyote anastahili hukumu,na ikiwa imejiachilia,basi itafika kwenye aibu na uharibifu.Mwanadamu hana haki ya kutaka kuwa kama malaika,kwa sababu hajakaribishwa kuwa katika ngazi hiyo,na hata malaika hana haki ya kutaka kuwa kama mwanadamu,kwa sababu hajapewa haki hiyo.

Ilikuwa matarajio ya kiburi cha Shetani ambacho kilileta unyanyashaji wake.na utaisha katika uharibifu wake. ( ***Isa.14:14***) “Kwa maana kila ajikwezaye atadhiliwa,naye ajidhiliye atakwezwa.” (***Luka 14:11***),lakini siyo lazima kwa ngazi ya juu..

Kwa sehemu kutoka kwa dhana ya uongo ya haki,na kwa sehemu kutoka kwa sababu nyingine,suala la uchaguzi kama lilivyofundishwa katika Maandiko limekuwa tukio la mgogoro na kutoelewana sana.Kwamba Maandiko yanafundisha uchaguzi ambao wachache hawawezi kukataa,lakini kwa kanuni ambayo uchaguzi umewekwa ni suala ambalo linatofautiana kimawazo,wengine wanadai kwamba ni uchaguzi unaofanywa kiholela,yaani usio na masharti,na wengine wanasema kwamba una masharti.Twaamini kwamba kuna kipimo cha ukweli katika pande hizi mbili za mitazamo hii.Uchaguzi wa sehemu ya Mungu ni onyesho la uamuzi wake kwa kusudi lake,kwa ofisi au hali.Mungu ameteua au kuchagua kwamba baadhi ya viumbe vyake wawe malaika,na wengine wawe watu,ili wengine pia wawe wanyama ,ndege,wadudu,n.k., na uchaguzi huo unapaswa uwe wa asili ya utukufu.Na japo Mungu anachagua kulingana na masharti fulani wote watakaopewa asili ya kiungu,lakini hatuwezi tukasema kwamba hawa wanastahili kuliko wengine;kwa sababu ni kwa neema kwamba kila kiumbe awepo katika ngazi aliyowekewa.

"Si katika uwezo wa yule atakaye,wala wa yule apigaye mbio;bali wa yule arehemuye,yaani Mungu” –fadhili au neema.( ***Warumi 9:16***).Sio kwamba waliochaguliwa walikuwa bora kuliko wengine,ndio maana Mungu aliwaita katika asili ya kiungu,kwa sababu aliwaacha malaika

ambao hawakutenda dhambi na akawaita baadhi ya wenye dhambi waliokombolewa kwa heshima ya utukufu.Mungu ana haki ya kufanya apendavyo na watu wake;na anachagua kutenda haki hiyo kwa kukamilisha mipango yake.Kwa hivyo kile tunacho ni neema ya utukufu, “Wewe ni nani umjibuye Mungu? Je! Kitu kilichoumbwa kimwambie yeye aliyekiumba,Kwani kuniumba hivi? Au mfinyanzi je! Hana amri juu ya udongo kuumba chombo kimoja kiwe cha heshima,na kimoja kikose heshima?” –au heshima kidogo? ( ***Warumi 9:20,21***).Wote waliumbwa na nguvu za kiungu-wengine wawe na asili ya juu na heshima kubwa,na wengine kuwa na asili ya chini na heshima ya chini.

"BWANA,Mtakatifu wa Israeli,na Muumba wake,asema hivi;Niulize habari za mambo yatakayokuja;mambo ya wana wangu,na habari za kazi ya mikono yangu;haya! Haya niagize.Mimi nimeumba dunia,nimemhuluku mwanadamu juu yake;mimi,naam,mikono yangu mimi,imezitanda mbingu,na jeshi lake lote nimeliamuru.” “ Maana BWANA,aliyeziumba mbingu,asema hivi,Yeye ni Mungu,ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya;ndiye aliyeifanya imara;hakuiumba ukiwa,aliiumba ili ikaliwe na watu;Mimi ni BWANA,wala hapana mwingine.” (***Isa.45:11,12,18***).Hakuna mtu yeyote anayeweza kumwagiza Mungu.Ikiwa alisimamisha dunia,na ikiwa hakuiumba ukiwa,na akamfanya ikaliwe na wale waliorejeshwa,watu kamilifu,basi sisi ni nani tupate kuongea dhidi ya Mungu,na kusema kwamba si haki akibadilisha asili yetu na kutufanya kuwa wamiliki wa asili ya kiroho kama ya malaika au kama asili yake ya kiungu? Ni jinsi gani itapendeza kumwendea katika unyenyekevu kwa Neno la Mungu na “kumwuliza” kuhusu yale yanayokuja,kuliko “kuamuru” au kusisitiza kwamba lazima afanye matakwa na dhana zetu? Bwana,mwokoe mtumishi wake kutoka kwa dhambi za kiburi:dhambi hizo zisiwe na mamlaka juu yetu.Hakuna mtoto wa Mungu yeyote,twaamini,anaweza kumlazimisha Bwana kwa kujua,japo ni rahisi sana na bila kujua watu wengi wanaanguka katika kosa hilo.

Kizazi cha binadamu ni wana wa Mungu kwa kupitia uumbaji-yaani kazi ya mikono yake-na mpango wake akiwarejea umefunuliwa wazi katika Neno lake.Paulo anasema kwamba mtu wa kwanza (ambaye alikuwa mfano wa vile kizazi watakuwa wakati watakapokuwa wakamilifu) alikuwa duniani;na ukoo wake,ila tu Kanisa la Injili,ambao katika ufufuo watakuwa bado kama wanadamu,watakaokaa katika dunia. ( ***1 Wakorintho 15:38,44***) Daudi anatangaza kwamba binadamu aliuumbwa chini ya malaika,na akatukuzwa na utukufu,mamlaka,n.k. ( ***Zab.8:4-8***) Na Petro,Bwana wetu,na manabii wote tangia dunia ianze,wanatangaza kwamba uzao wa binadamu utarejeshwa kwa ule utukufu mkamilifu,na tena atakuwa na mamlaka juu ya dunia,kama vile wawakilishi wake,Adamu,alivyopewa mamlaka. *Matendo 3:19-21*

Hiyo ndiyo sehemu Mungu amechagua kuwapa ukoo wa wanadamu.Ni sehemu yenye utukufu ilioje! Fumba macho yako kwa dakika chache kwa matukio ya taabu na ole,uharibifu na huzuni ambavyo bado vinaendelea kwa ajili ya dhambi,na upige taswira ya njozi ya akili utukufu wa dunia timilifu.Hakuna doa lolote litazuia utulivu na amani katika jamii iliyokamilika;hakuna wazo ya huzuni,sio kuangalia au neno lolote;upendo,kufurahia kutoka kwa moyo,utokao kwa kila moyo hukutana na jibu katika moyo mwingine,na huruma utaweka alama wa kila tendo.Magonjwa yao hayatakuwepo tena,hakuna uchungu wowote,na hata kuoza kwokwote hakutakuwepo-na hata woga kwa mambo kama hayo.Tafakari taswira zote za afya

yatakayokuwa na uzuri wa maumbile ya mwanadamu na hali ambayo hujawahi kuona,na ujue kwamba watu wakamilifu bado watakuwa na upendo unaopita kiasi.Utakaso wa ndani na ukamilifu wa akili na maadili utaimarisha na kumtukuza kila uso unaong'aa.Familia zote za dunia zitakuwa hivyo;na wale walioomboleza wakililia watu wao waliokufa watafutwa machozi,wakati watakapogundua kazi ya ufufuo umekamilika. *Ufunuo. 21:4*

Na haya yatakuwa mabadiliko tu kwa familia ya wanadamu pekee.Tunapaswa kujua pia kwamba dunia,ambayo "iliumbwa ikaliwe " na wazao wa binadamu,itakuwa nzuri na ya kupendeza kwao,kama vile ilivyoonyeshwa katika paradiso ya Kiedeni,ambapo mwanadamu mwakilishi alikuwepo mara ya kwanza.Paradiso itarejeshwa.Dunia haitaleta miiba na makwekwe,na haitahitaji tena jasho la binadamu ili ilete mkate,lakini " dunia italeta mavuno yake kwa njia rahisi na ya kawaida." Nyika zitachipusha maji ya kunawiri" ; uumbaji wa wanyama wa viwango vya chini utakuwa kamilifu,watakuwa watumishi wenye nia na watiifu;asili na aina zake tofauti itawaita wanadamu toka pande zote ili kutafuta na kujua utukufu na nguvu na upendo wa Mungu;na mawazo na moyo utafurahia katika yeye.Tamaa isiyo na mwisho wa kuvumbua kitu kipya,ambayo iko sasa hii,siyo jambo la kawaida lakini ni jambo lisilo la kawaida,kwa sababu ya udhaifu wetu,na pia kwa sababu ya mazingira yetu ya sasa ambayo hayatoshelezi tamaa zetu.Si nia ya Mungu kwamba tung'ang'anie kitu kipya.Karibia kila kitu kwa Mungu ni cha zamani,na anafurahia kwa vitu vingi vya zamani na kamilifu.Kwa hivyo hata wanadamu watakuwa hivyo atakaporejeshwa katika sura ya Mungu.Mtu mkamilifu hatajua na kufurahia kamili,na kwa hivyo hatautaka utukufu wa kiumbe cha kiroho,kwa sababu ya asili mpya,kama vile samaki na ndege,kwa sababu hiyo hiyo,wanapenda na kufurahia asili yao na kuipa kipaumbele.Binadamu atamezwa na kunyakuliwa na utukufu ambao umemzingira katika kiwango hicho cha ubinadamu kiasi kwamba hatakuwa na hamu ya ,au upendeleo wa asili nyingine au hali nyingine kuliko zile alikuwa nazo.Mtazamo katika uzoefu wa sasa utaonyesha hii. "Itakuwa ngumu," kwa ugumu wowote,kwa wale matajiri wa ulimwengu huu kuingia katika Ufalme wa Mungu.Vitu vichache vizuri tunavyomiliki,hata chini ya utawala wa uovu na mauti,vinavutia kwa asili ya mwanadamu kiasi cha kwamba twahitaji usaidizi wa Mungu ili tuweke macho yetu na kusudi letu liangaze ahadi za kiroho..

Kwamba Kanisa la Kikristo,mwili wa Kristo,ni mpango wa kipekee wa kawaida wa Mungu kwa wanadamu,unadhihirika kutoka kwa maelezo kwamba uchaguzi wake uliamuliwa katika mpango wa utukufu kabla ya msingi wa ulimwengu ( ***Waefeso 1 :4,5***),ambapo kwa wakati huo Mungu aliona kuanguka kwa uzao wa binadamu kwa dhambi na pia akapanga awali utakaso na uwekeaji wakfu na utukuzaji wa darasa hili,ambalo,kwa awamu ya Injili,amekuwa akiwaita kutoka kwa ulimwengu ili wawe katika sura ya Mwana wake,ili wawe wamiliki wa asili ya kiungu na warithi sawasawa na Kristo Yesu wa Ufalme wa miaka elfu kwa kusimamishwa kwa haki ya wote na amani . *Warumi 8:28-31*

Hili laonyesha kwamba uchaguzi wa Kanisa ulikuwa katika sehemu ya mpango wa Mungu lakini ujue kwamba sio uchaguzi usio na masharti kwa watu fulani wa Kanisa.Kabla ya msingi wa ulimwengu Mungu alipanga kwamba kusanyiko fulani lapaswa kuchaguliwa kwa kusudi kwa wakati fulani-wakati wa awamu ya Injili.Wakati hatuwezi kuwa na shaka kwamba Mungu hangeweza kuona tendo la kila mshirika wa Kanisa,na kuona yule ambaye angestahili na kwa

hivyo kuunda washiriki wa “kundi dogo,” japo hii siyo njia ambayo Neno la Mungu linaeleza fundisho la uchaguzi.Haikuwa mawazo ya kutayarishwa kwa mtu binafsi ambayo mitume walitaka kufundisha,lakini kwamba darasa lilitangulia kwa kusudi la Mungu kujaza nafasi ya heshima,uteuzi ambao utakuwa juu ya hali ya majaribio makubwa ya imani na utiifu na dhabihu ya marurupu ya kidunia,n.k, hadi wakati wa kifo.Kwa hiyo kwa majaribu ya mtu binafsi,na kushinda kwa mtu binafsi,mshirika binafsi wa darasa lililopangwa hapo awali wanachaguliwa ama kukubaliwa kwa mibaraka yote na faida Mungu alizijalia kundi lake.

Neno “kutukuza” katika ***Warumi 8:30***,linatoka kwa neno la Kiyunani “*doxazo*”,linalomaanisha *kuheshimiwa*.Sehemu ambayo Kanisa limechaguliwa ni ile ya heshima kubwa.Hakuna mtu angefikiria kuhusu heshima ya namna hiyo.Hata Bwana wetu Yesu alialikwa kabla ya kufikiria heshima kama hiyo,kama tunavyosoma: “ Yesu pia alitukuzwa [doxazo-heshimika] sio yeye mwenyewe alijifanya kuwa Kuhani Mkuu,lakini yule aliyemwambia, “ Ndiwe mwanangu,Mimi leo nimekuzaa” Baba wa Mbinguni basi aliheshimu Bwana wetu Yesu;na mwili wa wateule ambao ni warithi pamoja na yeye wataheshimiwa na neema ya Yehova.Kanisa,kama vile Kichwa chake,wameanza kupitia “heshima” wakati wamezaliwa na Mungu kwa asili ya kiungu kupitia kwa neno la kweli (***Yakobo 1:18***),na wataingizwa kwa heshima wakati watazaliwa kwa Roho,yaani watakapokuwa viumbe vya kiroho-katika sura ya Kichwa ambaye ametukuzwa.Wale ambao Mungu atawaheshimu basi lazima wawe kamilifu na safi;na kwa vile tulikuwa wenye dhambi walizaliwa ndani ya dhambi,hakutuita na kutualika katika heshima pekee bali pia *alituhesabia haki* toka kwa dhambi kupitia kwa kifo cha Mwanawe,ili tupate heshima ambayo ilitufanya atuite.

Katika kuchagua kundi dogo,Mungu anatoa wito wa kawaida- “wengi wameitwa.” Sio wote wameitwa.Wito uliwekwa kwanza ,wakati wa huduma wa Bwana wetu,kwa Waisraeli wa mwili,lakini sasa ni kwa wengi waitwao na Mungu (***Luka 14:23***) wanapaswa kuhimizwa au kuzuiliwa (sio kulazimishwa) ili waje katika karamu ya kipekee ya neema.Lakini hata wale wanaosikia na kuja,wote hawastahili.Nguo za harusi (haki inayohesabiwa kwa Kristo) zinapeanwa lakini wengine hawatazivaa,na lazima wakataliwe;na wale wanaovaa kanzu ya halali ambao wamepokea heshima ya kuzaliwa kwa asili mpya,wengine wanakosa kufanya wito wao uwe wa haki kwa kuwa waaminifu kwa agano.Kwa wale wanaostahili kuonekana na Mwana Kondoo katika utukufu,basi inatangazwa hivi, “ *Wameitwa* na *kuchaguliwa* na ni *waaminifu.*” *Ufunuo. 14:1; 17:14*

Mwito ni wa ukweli;jitihada ya Mungu ya kuchagua na kuinua Kanisa haiwezi kubadilika; lakini wale ambao watakuwa katika kundi hilo watakuwa kwa kupitia masharti.Wale wote watakaoshiriki heshima iliyopangwa zamani lazima watimize masharti ya wito. “Basi,ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake,na tuogope,mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.” (***Waeb.4:1)***.Wakati neema kubwa sio kwa yeye anayetaka au kwa yeye akimbiaye;bali ni kwa yeye anayetaka na anayekimbia wakati aitwapo..

Kwa hiyo twaamini waziwazi kwamba inaonyesha haki ya Mungu na kusudi lake ili afanye mapenzi yake,tunasema kwa hakika kwamba kanuni ambayo inaonyesha upaji wa neema zote za Mungu kwa faida ya wote.

Basi,katika mamlaka ya Maandiko,tunatambua ukweli kwamba asili ya kibinadamu na kiroho ni tofauti na ya kipekee-kwamba kuweka pamoja asili mbili sio mpango wa Mungu,lakini itakuwa tu jambo lisilo kamili,na kwamba kubadilika kutoka kwa asili moja hadi nyingine sio sheria,lakini ni jambo lisilo kawaida,kama vile Kristo alivyofanyiwa-ni suala la kina ambalo linafaa lijulikane jinsi mabadiliko yanakamilishwa,na katika hali gani yanafaa kufikiwa na kwa njia gani yatafanyika. .

Hali ambazo Kanisa linaweza kutukuzwa na Bwana wake kufikia asili ya Kiungu ( ***2 Pet.1:4***) ni sawa na hali ambazo alizipokea utukufu huo;na kuzifuata nyayo zake ( ***1 Pet.2:21***)),akijitoa kama dhabihu iliyo bora,kama alivyofanya,na baadaye kutekeleza kiapo cha uwekeaji wakfu hadi dhabihu ilipokomaa wakati wa kifo chake.Kubadilika kwa asili kutoka kwa asili ya binadamu hadi asili ya uungu kutapeanwa kama ujira kwa wale ambao,kwa awamu ya Injili,wamejitoa kama dhabihu *asili ya kibinadamu*,kama vile Bwana wetu alivyofanya,pamoja na tamaa zake,matumaini na malengo,ya sasa na za usoni-hata wakati wa kifo.Katika kiyama wataamka,sio tu kushiriki na watu wengine katika kuwekwa kwa binadamu kuwa wakamilifu na mibaraka inayofuatia,lakini pia watashiriki katika sura na utukufu na furaha wa Bwana,kama warithi na yeye wa tabia ya Uungu.. *Warumi. 8:17*; *2 Tim. 2:12*

Mwanzo na ukuzaji wa asili mpya zimefananishwa na mwanzo na ukuzaji wa uhai wa binadamu.Kwa upande moja,kuna kusababisha na baadaye kuzaa,kama pia kwa upande mwingine.Watakatifu wanasemekana kwamba wamesababishwa na Mungu kupitia kwa Neno la kweli. ( ***1 Pet.1:3;1 Yohana 5:18;Yakobo 1:18***).Ina maana kwamba wanapokea pumzi mara ya kwanza katika uhai wa kiungu kutoka kwa Mungu kupitia kwa Neno.Wakati wamefanyiwa haki bure kupitia kwa imani katika fidia,wanasikia wito, " Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai,takatifu, [ya kutolewa fidia,uliowekwa wakfu,na baadaye] ya kumpendeza Mungu,ndiyo ibaada yenye maana." (***Warumi 12:1***); na wakati,katika kutii wito huo,wanajitakasa kabisa ubinadamu wao kwa Mungu,kama dhabihu iliyo hai,sako kwa bako na ya Yesu,na Mungu anakubali;na kwa tendo hilo uzima wa kiroho unaanza.Watu kama hao wanajipata wakifikiri na kuongozwa wakifanya kama wenye mawazo mapya (yaliyobadilika),hadi wakati wa kusulubiwa kwa asili yao ya kibinadamu.Kutoka kwa wakati ule wa kutakaswa, Mungu anawatambua kama "viumbe vipya."

Kwa hiyo *viinitete* vya "viumbe vipya" mambo ya kale [ tamaa ya binadamu,matumaini,mipango,n.k] yanapita,na mambo yote yanakuwa mapya.Kiinitete ya "kiumbe kipya" kinaendelea kukua na kuendelea,kama vile asili ya kale,pamoja na matumaini yake,malengo,tamaa,n.k., inasulubishwa.Michakato hii miwili inaendelea taratibu.kutoka kwa wakati utakaso unaanza hadi kwa binadamu na kuzaliwa kwa tokeo la kiroho.Wakati Roho wa Mungu anaendelea kuonekana,kupitia kwa Neno lake,mipango yake mingi,anaanza basi kuharakisha hata miili yetu inayoharibika (***Warumi 8:11***),na kuwezesha miili hii yetu kumfanyia huduma;lakini muda usio mrefu tutakuwa na miili mipya-ya kiroho,kibingu, ambayo imetengenezwa kwa njia yoyote kuwa mipya,na kuwa na mawazo ya uungu.

Kuzaliwa kwa "kiumbe kipya" kunafanyika wakati wa ufufuo ( ***Wakol.1:18***); na ufufuo wa kundi hili umetajwa kama wa kwanza ( au wa waliochaguliwa). ***(Ufunuo 20:6***).Twapaswa kukumbuka kwamba sisi si viumbe vya kiroho hadi wakati wa ufufuo,japo wakati tunapokea

roho wa kufanywa wana tunahesabiwa kuwa wa kiroho. (***Warumi 8:23-25;Waef.1:13,14;Warumi 6:10,11***).Wakati tumekuwa viumbe vya kiroho hasa,yaani,wakati tumezaliwa na Roho,hatutakuwa tena na mwili wa nyama na damu,kwa sababu "aliyezaliwa na Roho ni roho."

Kuzaliwa kwa asili ya kiroho katika ufufuo lazima inafuatwa na kusababishwa kwa Roho katika utakaso,kama vile kuzaliwa kwa mwili kunafuatwa na mwili.Wote waliozaliwa na mwili katika mfano wa Adamu wa kwanza,wa kidunia,walisababishwa na mwili;na wengine wamesababishwa tena na Roho wa Mungu kupitia neno la kweli,ili kwamba wakati unaokuja wazaliwe na Roho katika mfano wa mbingu,katika ufufuo wa kwanza: " Na kama tulivyoichukua sura yake yule wa udongo,kadhalika [Kanisa] tutaichukua sura yake yeye aliye wa mbinguni"-ila tu tukianguka . *1 Wakor. 15:49*; *Waeb. 6:6*

Hata kama kukubali  wito wa mbinguni na utakaso wetu katika utiifu wake unaamuliwa kwa wakati fulani,kuleta kila wazo katika makubaliano na mawazo ya Mungu ni kazi itakayofanyika kwa utaratibu ambao unaelekea kwa tabia ya kibingu kutoka kwa taratibu inayoelekea kidunia.Mtume anaeleza mchakato wa kazi hii ya mabadiliko,akisema, "Wala msifuatishe namna ya dunia hii;bali mgeuzwe kwa kufanywa upya [kwa asili ya kibingu] nia zenu,mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema,ya kumpendeza,na ukamilifu."  *Warumi 12:2*

Twapaswa kujua kwamba maneno haya ya Mtume hayajatajwa kwa ulimwengu usioamini,lakini kwa wale ambao anawatambua kama wapendwa,kama inavyoonyeshwa na mstari uliotangulia- " Basi,ndugu zangu,nawasihi,kwa huruma zake Mungu,itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai,takatifu,ya kumpendeza Mungu."

Inaaminika kwamba wakati mtu amebadilika na amegeuka kutoka kwa dhambi na kuingia kwenye haki,na kutoka kwa kutoamini na kupinga Mungu na kuanza kumtegemea Mungu,hapo basi amepata mabadiliko ambayo Paulo alimaanisha . Kwa kweli ni mabadiliko makuu-mgeuzo ,lakini sio mgeuzo ambao Paulo alikuwa akitaja.Huo ni mgeuzo wa tabia,lakini Paulo alikuwa akitaja mgeuzo wa asili ambao uliahidiwa waumini wakati wa awamu ya Injili,kupitia kwa masharti,na alikuwa akiwahimiza waumini kuyatimiza masharti  hayo.Kama  mgeuzo kama huo wa tabia ungekuwa umefanyika kwa wale  aliowataja,hangewaita wapendwa-wapendwa,pia,ambao pia walikuwa na kitu kilichokuwa "takatifu na kumpendeza" Mungu" ili watoe kama dhabihu;kwa sababu wale tu waliotakaswa kwa imani katika fidia ndio wanahesabiwa  na Mungu kama watakatifu na kumpendeza.Mgeuzo wa asili unaleta,kwa wale ambao katika awamu ya Injili,wamejitoa utu wao uliotakaswa kama dhabihu iliyo hai,,kama vile Yesu alivyojitoa utu wake mkamilifu kama dhabihu,akiwacha haki yote na madai kwa kuwepo kwake nyakati za usoni,na hata pia akikana mapendekezo ya binadamu, faida,haki,n.k.Kitu cha kwanza cha kutoa kama dhabihu ni nia ya binadamu;na baadaye hatuwezi kuongozwa na nia yetu au nia ya binadamu,bali kwa nia ya Mungu.Nia ya Uungu ndiyo itakuwa nia yetu,na tunatambua nia ya binadamu kama si nia yetu,lakini kama nia ya mwingine,ambayo inatakikana ipuuzwe na kutolewa kama dhabihu.Baada ya nia ya Uungu kuwa kama nia yetu,tunaanza kuwaza,kutoa hoja na kuhukumu kwa njia ya kiungu:Mpango wa Mungu unaanza kuwa mpango wetu,na njia za Mungu zinaanza kuwa njia zetu.Hakuna mtu anayeweza kuelewa mgeuzo huo ambaye kwa imani nzuri hajajitoa kama dhabihu iliyo bora,na baadaye kuyaona matokeo

yake.Awali twaweza kufurahia chochote ambacho kwa hakika siyo dhambi;kwa sababu ulimwengu na vitu vizuri vilivyomo viliumbwa ili mwanadamu afurahie,ugumu ni kudhibiti mielekeo ya dhambi.Lakini waliotakaswa,na kugeuzwa,kwa jitihada ya kupunguza dhambi,lazima wajitoe kama dhabihu ya vitu vizuri na kuweka nguvu zao zote kwa huduma ya Mungu.Na wale wote walio waaminifu katika huduma na kujitoa watagundua hakika kila siku kwamba ulimwengu huu sio mahali pao pa kupumzika,na kwamba hapa hawana mji unaodumu.Lakini mioyo yao na matumaini yao yatageuzwa kwa "pumziko linalosalia kwa watu wa Mungu." Na tumaini lililobarikiwa litafika haraka na kutia msukumo dhabihu iendelee.

Kwa hiyo,kupitia kwa utakaso,mawazo yanakuwa mapya na kugeuzwa,na tamaa,matumaini na malengo yanaanza kugeukia vitu vya kiroho na visivyoonekana ambavyo viliahidiwa,wakati matumaini ya binadamu n.k., yanakufa.Wale ambao wamegeuzwa,ama wako katika mchakato wa kubadilishwa wanatambulika kama " viumbe wapya," ambao wamezaliwa na Mungu,na warithi kwa kiwango cha asili ya Mungu.Marko anatofautisha kati ya "viumbe wapya" na wale waumini na " wapendwa" ambao wametakaswa.Wale wa kutakaswa bado wako duniani,wako na tabia ya dunia,na mbali na tamaa zao za dhambi,matumaini yao,matarajio,na malengo yao yatainuliwa wakati ulioahidiwa wa kufanya upya vitu vyote.Lakini wale wa kikundi cha kwanza sio wa ulimwengu huu kama Kristo pia sio wa ulimwengu huu,na matumaini yao yanaangazia mambo yasiyoonekana,mahali ambapo Kristo anakalia katika mkono wa kuume wa Mungu.Matarajio ya utukufu wa kidunia,ambao unavutia sana kwa binadamu wa kawaida,hautakuwa sehemu ya wale waliozaliwa kwa tumaini la kibingu,kwa wale wanaoona utukufu wa ahadi za kibingu,na watakaofahamu sehemu ambayo wamewekewa katika mpango wa Mungu.Mawazo haya mapya ya kiungu ndiyo jitihada ya urithi wetu,mwili mtakatifu;-mawazo na mwili.Wengine wanaweza kuduwazwa na semi mwili wa uungu lakini twaambia kwamba Yesu ndiye mfano halisi wa Baba,na kwamba washindi watakuwa "kama yeye na kumwona jinsi alivyo." (***I Yohana 3:2***) "Kunao mwili wa kawaida wa binadamu,na kuna wa kiroho. (***I Wakorintho 15:44***),Hatungefikiri kwamba Baba yetu au Bwana wetu mkuu Yesu alikuwa na mawazo makuu bila miili.Kuna miili ya kiroho iliyotukuzwa,japo haijaonekana namna ya huo utukufu,na hautaonekana hadi wakati tutakaposhiriki katika utukufu huo.

Wakati mgeuzo huo wa mawazo kutoka kwa binadamu hadi kiroho ni kazi inayofanyika kwa utaratibu,mabadiliko kutoka kwa mwili wa binadamu hadi mwili wa kiroho hautakuwa polepole,lakini papo na hapo. ( ***1 Wakorintho 15:52***).Basi,kama vile Paulo anavyosema,tunao hazina (wazo la Uungu) katika vifaa vya udongo,lakini hivi karibuni hazina itakuwa ndani ya kifaa ambacho kinamtosha-yaani mwili wa Kristo.

Tumeona kwamba asili ya binadamu iliumbwa kwa mfano wa tabia ya kiroho. ***( Mwanzo 5:1***).Kwa mfano,Mungu ana nia,pia wanadamu na malaika;Mungu ana akili na kumbukumbu,na hata viumbe vyake wenye akili-malaika na watu.Tabia ya shughuli za akili ya kila mmoja ni sawa.Japo twajua kwamba viwango vya kiroho vina nguvu zaidi ya wanadamu,-nguvu ambazo zinaleta,kama vile tunavyofikiri,hazitoki kwenye viwango tofauti,lakini zatoka kwa viwango mbalimbali na hali ambazo zinafanya kazi.Asili ya binadamu ni sura kamili ya asili ya kiroho,ambayo ina viwango sawa,lakini imefungamana kwa eneo ya kidunia,na kwa uwezo na

mamlaka ya kutambua kwa njia ya pekee zaidi ya vile Mungu alivyofunua kwa faida ya binadamu na furaha yake.

Uungu ndio kiwango cha juu ya asili ya kiroho;na kuna umbali zaidi kati ya Mungu na viumbe vyake! Twaweza tu kupata mianga michache ya utukufu wa hekima ya Uungu,nguvu na uzuri kama katika mtazamo wa mandhari yote ambayo yanasababisha baadhi ya kazi zake kuzipitia mbele zetu.Lakini twaweza kupima na kufahamu utukufu wa ubinadamu ulio kamilifu.

Na mawazo haya yote yakiwa katika akili,twaweza kufahamu jinsi mabadiliko kutoka kwa asili ya binadamu hadi kwa asili ya kiroho yanafanyika,k.v., kubeba nguvu sawa ya akili hadi hali ya juu.Wakati tutavalishwa na mwili wa mbinguni,tutakuwa na nguvu za kibingu ambayo ni ya mwili wa utukufu;na tutakuwa na mawazo na upana wa nguvu ambayo ni ya mwili huo,

Mabadiliko au mgeuzo wa mawazo,kutoka kwa mwili wa kidunia hadi mwili wa kibingu,ambayo waliotakaswa watapata hapa,ndiyo mabadiliko ya asili.siyo mabadiliko ya ubongo,ama mwujiza ya kufanyika kwake,lakini ni nia na kubadilishwa kwa mawazo ndiyo yanabadilika.Nia yetu na matamshi yetu ndio yanawakilisha ubinafsi wetu;kwa hiyo tunabadilishwa,na hakika tunahesabiwa kama walio wa asili ya kibingu,wakati nia na matamshi yetu yamebadilishwa.Ni kweli kwamba ni mwanzo mdogo;lakini ni kusababishwa,vile linaitwa,mara nyingi ni mwanzo mdogo;japo ni juhudi au uhakika ya kazi inayomalizika . *Waefeso 1:13,14*

Wengine wameuliza,twaweza kujijua namna gani tutakapobadilishwa? Tutajuaje kwamba sisi ndio wale ambao waliishi na kuteseka na kujitoa kuwa washiriki wa utukufu? Je tutakuwa wale viumbe wanaofahamu kilichotendeka? Hakika,ndiyo.Tukiwa tumekufa na Kristo,tutaishi pia pamoja naye.(***Warumi 6:8***).Mabadiliko yanayofanyika kila siku kwa miili yetu ya binadamu hayafanyi tusahau yaliyopita,ama kupoteza utambulisho wetu.*

---

**Miili yetu ya binadamu inazidi kubadilika.Sayansi inasema kila miaka saba inashuhudia mabadiliko kamili katika sehemu za atomu yetu.Kwa hivyo mabadiliko yaliyoahidiwa kutoka kwa miili ya kibinadamu hadi miili ya kiroho hayataharibu kumbukumbu au utambulisho,lakini yataongeza nguvu na upeo.Tutakuwa na mawazo ya kiungu ambayo yatakuwa yetu,na kumbukumbu ile,pamoja na nguvu za kutoa hoja n.k.,itakuwa kwamba nguvu zake zitaongezeka kwa upana na marefu,kwa mujibu wa mwili wake mpya wa kiroho;na kumbukumbu itaelezea kazi yetu yote kutoka utotoni mwetu,na tutaweza kulinganisha na kutambua kamili thawabu ya kujitoa kwetu.Ni hii hainhgekuwa ikiwa binadamu hangekuwa mfano wa kiroho.*

---

Haya mawazo pia yanaweza kutusaidia kuelewa jinsi Mwana pia,wakati alibadilishwa kutoka kwa hali za kiroho hadi kwa hali za binadamu-yaani kwa asili ya binadamu na mapungufu ya kidunia-alikuwa mtu;hata hivyo alikuwa kiumbe kwa hali mbili,chini ya hali za kwanza alikuwa kwa mwili wa kiroho na chini ya hali ya pili alikuwa binadamu.Kwa sababu asili mbili hizi ni

zinatengana na ni tofauti,na japo moja inafanana na nyingine,kwa hivyo,viwango sawa ya akili (kumbukumbu,n.k.) ambazo zinafanana kwa pande zote,Yesu angaweza basi kugundua utukufu wake wa awali aliyekuwa nao kabla ya kuwa binadamu,na ile asiyekuwa nayo kabla ya kuwa binadamu,na maneno yake yanathibitisha akisema- “Na sasa,Baba,unitukuze mimi pamoja nawe,kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe,kabla ya ulimwengu kuwako.” (***Yohana 17:5***)-utukufu wa asili ya kiroho.Na sala imejibiwa zaidi katika utukufu wa hali ya juu ya aina ya kiumbe wa roho,yaani asili ya kiungu.

Ukirejelea tena maneno ya Paulo,twagundua kwamba hasemi tusifuatishe namna ya ulimwengu huu bali mgeuzwe  kwa kubadilishwa kwa mfano wa uungu;bali anasema, “msifuatishe namna ya ulimwengu bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu” Hii imeelezwa vizuri,kwa sababu hatufuatishi au kujigeuza peke yetu;bali tunajitoa peke yetu kufuatisha ulimwengu na ushawishi wake,roho ya ulimwengu unaotuzingira,au tunajitoa kwa mapenzi ya Mungu,mapenzi matakatifu au Roho,ili tugeuzwe na ushawishi wa kibingu ambao unafanywa kupitia kwa Neno la Mungu.Wewe ambaye umetakazwa,unajitoa kwa ushawishi gani? Ushawishi wa mgeuzo unaongoza kwa kujitoa na kuteseka,lakini mwisho wake una utukufu.Ikiwa unazidi kuwa chini ya ushawishi huu,unathibisha kila siku hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema,ya kumpendeza,na ukamilifu.

Wacha wote ambao wameweka kila kitu katika madhabahu ya kujitoa kila mara wajue kwamba,wakati Neno la Mungu linabeba ahadi za kidunia na za kibingu,yetu ni za kibingu.Hazina yetu imo mbinguni:wacha mioyo yetu izidi kuwa huko.Wito wetu sio kuwa na asili ya kiroho pekee,lakini kuwa katika kiwango cha juu cha kiroho,asili ya kiungu- “bora kuliko malaika.” ( ***2 Pet.1:4;Waeb.1:4***).Wito huu wa kibingu umeshikamana na awamu ya Injili:Hukufanywa kabla ya awamu hii,na utaisha wakati wa mwisho wa awamu hii.Wito wa dunia ulifanywa,hata hivyo watu hawakupata kuelewa kikamilifu,kabla ya wito wa mbinguni,na tunaambiwa kwamba utaendelea baada ya awamu ya Injili. Maisha [kwa wale ambao wamerejeshwa kama wanadamu] na kutokufa [ tuzo ambayo mwili wa Kristo unaendeshwa] zote zimeelezwa zote katika awamu hii. ( ***2 Tim.1:10***).Asili zote za binadamu na za kiroho zitatukuzwa katika ukamilifu,japo zinatengana na ni tofauti.Hakuna kipengele cha utukufu wa kazi iliyokamilika ya Mungu itakuwa ya aina nzuri,japo itakuwa ya maelewano makubwa,ya vitu vyote,vilivyo na akili na visivyokuwa na akili-wakielewana na kila mmoja na pia walielewana na Mungu.

Kanisa la Mungu

"Sayuni,inuka,ukaanze kuimba kwa furaha ya milele;
Sifa za Mungu zadumu milele,
Ambaye maadui wake huharibu

Wewe Kanisa la Mungu amkeni! Amkeni!.
Ambaye mihimili ya mwanga wake hutoka juu;
Toka ardhini na mavumbini nguo zake zatetemeka,
Utukufu wake u karibu.

"Ili aiunuliwe juu ya nchi,
Mungu kwa nguvu yake atatenda;
Atageuza maombolezo yake yawe furaha,

Huzuni yako itakuwa furaha.
Katika safu zinazoangaza,
Safisha nguo zake;
Mfalme wako atakuongoza kwenye njia
Takatifu,salama na hakika."